TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

26th AUGUST 2021

ELIMU KWA MTOTO WA KIKE NA NAFASI YA KURUDI SHULENI BAADA YA KUJIFUNGUA

TEN/MET ni mtandao wa kitaifa unaojumuisha mashirika yasiyo ya kiserikali 140 yanayojishughulisha na elimu hapa nchini. Lengo kuu la mtandao ni kuhakikisha kila mtoto wa kitanzania anapata haki yake ya kimsingi ya elimu msingi. Kwa miaka kadhaa, mtandao umekuwa ukiunga mkono jitihada za serikali, kuhakikisha kuwa kuna usawa wa kijinsia kwenye upatikanaji wa elimu kwa asimilia 50 kwa 50.

Katika lengo la kuhakikisha kunakuwa na usawa wa kijinsia kwenye upatikanaji wa elimu, TEN/MET imefanikiwa kufanya utafiti ili kubaini ufanisi, changamoto na uwezo wa vituo vya elimu kwa njia mbadala (alternative education pathways) vinavyoweza kumuandaa na kumsaidia mtoto wa kike aliyelazimika kuacha shule kwa sababu ya ujauzito ili kuweza kutimiza ndoto zake kimaisha. Kulingana na utafiti huu, tumefahamishwa kuwa;

I. Vituo vingi vinavyotoa elimu kwa njia mbadala vinapatikana maeneo ya mjini na sio vijijini, hivyo watoto wengi waishio vijijini hukosa fursa ya kujiunga.
II. Pia vituo hivi ili kujiunga kuna gharama ambayo mwanafunzi pamoja na mzazi/mlezi wake lazima wa ghramie ikiwemo, ada, malazi, chakula, usafiri, sare za shule na mengineyo. Hii hupelekea watoto wengi wanaotoka kwenye mazingira magumu ya kimaisha kushindwa kujiunga na vituo hivi.
III. Hatuna sheria ama sera mahususi inayoongelea mtoto akipata ujauzito akiwa shuleni anatakiwa kufukuzwa shule. Uachishwaji wa shule umekuwa ni mapokeo na tafsiri ya Sheria ya Elimu 1978 iliyofanyiwa marekebisho 2002- kifungu cha sheria namba 4 kinachosema (nanukuu kwa kiingereza)

“The expulsion of a pupil from a school may be ordered where:

b) The pupil has committed a criminal offence such as theft, malicious injury to property, prostitution, drug abuse or offence against morality whether or not the pupil is being or has been prosecuted for an offence.”.

Hivyo binti akipata ujauzito anafukuzwa kwa tafsiri ya sheria hii kuwa amefanya kosa la kimaadili (offense against morality).

Aidha utafiti huu umekuja na mapendekezo matano kati ya hayo ni;

I. Serikali ifanye mapitio ya Sheria ya elimu 1978, ilikuongeza kipengele cha mtoto wa kike akipata ujauzito arudi shuleni kwa njia ya mfumo rasmi mara tu atakapojifungua au kuwa tayari kurejea kwenye masomo yake.
II. Tafiti pia imebaini kuwa, kuna asilimia 78 ya watoto wa kike waliofukuzwa shule dhidi ya ujauzito hawatamani tena kurudi shule, hivyo tuiombe serikali ihimarishe vituo hivi ili kumuwezesha mtoto huyu kujiunga bila gharama au kwa gharama nafuu sana kama ilivyo kwenye elimu msingi.

Aidha, TEN/MET inatambua kuwa mwezi Mei mwaka huu (2021), Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, aliwataarifu waandishi wa habari wakati alipotembelea shule ya Sekondari Kibasila akiambatana na Waziri wa Uingereza anayeshughulikia maswala ya Afrika, ambapo alisema kuwa; kupitia fedha za Benki ya Dunia (World Bank) fedha za kimarekani million 500 ($500 million) kuna fungu limetengwa kuhakikisha mtoto aliyeachishwa shule kwa ajili ya ujauzito atakapo faulu kupitia elimu ya njia mbadala/mfumo usio rasmi basi ataweza kurudi kwenye mfumo rasmi na kupangiwa shule za serikali. Sisi kama wadau tunapongeza sana serikali kwa jitahada hizi lakini utafiti wetu umetujulisha kuwa **umbali mrefu na gharama** ya kujiunga kwenye mfumo wa elimu mbadala umekuwa ni kikwazo cha watoto wa kike kujiunga. Pia taarifa hii ya kifursa haijaweza kuufikia uma kwa mapana ili kutambua fursa hii mbadala ingawa ina changamoto zake

Lakini pia, sisi kama mtandao tumechukua jukumu la kukutanisha wadau wa elimu kutoka kila pembe ya nchi kwa siku mbili mfululizo (tarehe 25 na 26 Ogosti) tukiwa na lengo la kuangaza ni namna ipi sahihi ya kumsaidia mtoto wa kike aliyekatishwa masomo kwasababu ya ujauzito na kunyimwa nafasi ya kurudi tena kwenye mfumo rasmi wa elimu hadi apitie kwanza kwenye mfumo usio rasmi ambao pia una gharama na haupatikani kwenye kila wilya na ngazi ya mkoa.

Aidha maoni ya wadau hawa ni;

1. Kuna umuhimu wa sera, sheria na miongozo yetu ya elimu kumpa nafasi ya kurudi shuleni msichana aliyekatishwa masomo kwasababu ya ujauzito. Hii ni kwasababu, Tanzania imesaini maridhiano kadhaa ya kimataifa ili kuhakikisha kuna upatikanaji wa elimu bora na yenye kuzingatia usawa wa kijinsia. Lakini pia hatutakiwi kuwa na sheria ambazo ni kandamizi, zinazokinzana na zisizojali haki za watu kwa ujumla.

2. Kulingana na tafiti mbali mbali zilizofanywa na wadau wa elimu, imebainika kuwa sababu ya wanafunzi kupata ujauzito sio “kimbelembele”, “uhuni” au “kujitakia” kama inavyosemekana na kudhaniwa na watu wengi, bali ni umaskini uliokithiri hivo kupelekea wao kudanganyika kwa vizawadi vidogovidogo, umbali kutoka shule ambapo njiani hukumbana na vishwawishi vingi, ubakaji, ndoa za kulazimishwa na ukosefu ya afya ya uzazi na jinsia.

Hivyo, tunaiomba serikali yetu sikivu ya awamu ya sita kuangalia swala hili kwa jicho pana na yakinifu kwani matokeo ya hili ni kuendeleza umasikini uliokithiri na kuongeza wimbi la wanawake wasio na elimu nchi na hivyo kuwa kikwazo cha kuweza kufikia malengo ya kidunia ya kufikia usawa wa kijinsia mnamo mwaka 2030.

ASANTE

Imetolewa kwenu na TEN/MET